**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA CHUNYA**

Tarehe. 20 /01/2026

# Yah: TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA MUDA MFUPI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya anawatangazia wananchi wenye sifa za kujaza nafasi za Ajira Ualimu ya Muda (Vibarua) katika Shule ya Awali na Msingi ya Mchepuo wa Kiingereza **(CHUNYA PRE & PRIMARY ENGLISH MEDIUM).**

*Nafasi za Ualimu zinazohitajika* **5**

**Ngazi ya Stashahada 2**

**Ngazi ya Shahada 3**

## SIFA ZA MWOMBAJI

1. Awe Raia wa Tanzania mwenye akili timamu
2. Awe na Umri kuanzia miaka 18 - 45
3. Awe na Ujuzi wa kutumia Tanakirishi (Computer)
4. Awe na Elimu ya Stashahada au Shahada ya Ualimu
5. Awe na Umahili wa kuongea Lugha ya kiingereza kwa Ufasaha
6. Awe Mwaminifu na Muadilifu

## MASHARITI YA JUMLA KWA WAOMBAJI

1. Ajira hizi ni za Mkataba wa miezi mitatu. Ambapo kuongezewa mkataba utategemea na ufanisi wako wa kazi.

CamScanner

2. Mwajiriwa wa Ngazi ya Stashahada atalipwa mshahara wa Tsh. **300,000/=** kwa mwezi na Mwajiriwa Ngazi ya Shahada atalipwa Mshahara **Tsh 400,000/=**

3. Mwombaji atafanya kazi katika shule ya **CHUNYA ENGLISH MEDIUM**

4. Mwombaji anatakiwa aambatanishe nakala za vyeti vyake vya shule na taaluma, Cheti cha kuzaliwa, pamoja na Wasifu binafsi (CV) na "Passport size" (2) zilizopigwa hivi karibuni.

5. Barua zote ziwe na anuani sahihi ya mwombaji pamoja na namba za simu zinazopatikana muda wote.

6. Kuwasilisha taarifa za uongo/kughushi nyaraka ni kosa la jinai. Hivyo atakayebainika kutenda kosa hilo hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

7. Maombi yote yatumwe kwa anuani ya:-
   Mkurugenzi Mtendaji (W),
   Halmashauri ya Wilaya ya Chunya,
   S. L. P. 73,
   **CHUNYA.**

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 26/01/2026 saa 9:30 Alasili

Imetolewa na

Tamim H. Kambona

**MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA,**

**CHUNYA.**

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
CHUNYA

CamScanner